# Baadhi ya Vipengele vya Uambatizi wa Vitenzi katika Kishambala

**Rhoda Peterson**

**Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**Ikisiri**

Uambatizi ni mchakato mmojawapo wa kimofolojia unaohusu uundaji wa maneno. Mchakato huu huhusisha kategoria mbalimbali za maneno, kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, vimilikishi, na vioneshi (Kiango, 2000). Vipengele mbalimbali ndani ya kategoria hizo huweza kutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine kutegemeana na sarufi ya lugha husika. Lengo la makala hii ni kuchunguza na kudhihirisha jinsi baadhi ya vipengele vya uambatizi wa vitenzi vinavyojitokeza katika Kishambala. Uchunguzi huu mdogo ni sehemu ya uchunguzi mpana unaolenga kuchambua sarufi ya Kishambala, kazi iliyoanzwa na wataalamu kadhaa, mmojawao akiwa marehemu Prof. Besha (1985).

## 1.0 Utangulizi

Nduni mojawapo ya mofolojia kama kipengele cha isimu ni kuruhusu uambikaji wa viambishi katika ma neno. Viambishi hivi hubeba dhana mbalimbali k.m. njeo, nafsi, urejeshi, utendea, utendwa, usababishi n.k. Uambikaji uko wa aina mbili; uambatizi na unyambulishi. Uambatizi huhusisha viambishi ambavyo huunda maumbo tofauti ya leksimu moja. Maumbo haya hayabadili maana wala kategoria ya neno, bali huongeza nduni za kisarufi tu katika neno husika (Bauer, 1988; Spencer, 1991; Katamba, 1993; Kiango, 2000). Kwa mfano, tukitumia kitenzi cha Kishambala *'toa'* (piga), maumbo mengine yanayohusiana na kitenzi hiki yanaweza kuundwa k.m. *a-a-toa* (anapiga), *na-a-toa* (ninapiga), *wa-a-toa* (wanapiga), n.k.

Viambishi vilivyopigiwa mstari ni viambatizi kwani uambikwaji wake haubadili maana au kategoria ya neno *'toa'*. Katika kitenzi *a-a-toa, a-* ya mwanzo huonesha nafsi ya tatu umoja na ya pili njeo iliyopo. *Na-* katika kitenzi *na-a-toa* huonesha nafsi ya kwanza umoja na *-a-* huonesha njeo/ wakati uliopo. *Wa-* katika kitenzi *wa-a-toa* huonesha nafsi ya tatu uwingi na *-a-* njeo/wakati uliopo. Upachikaji wa viambishi ambatizi huukiliwa na sintaksia. Kwa mfano, kwa kutumia sentensi *'Ngwana aaja mghua'* (Mtoto anakula muwa), utokeaji wa kiambatizi *a-* cha mwanzo katika neno *'aaja'* hutegemea hadhi ya nomino iliyotangulia. Nomino hiyo ina kiambishi *ngw* kinachorejelea *umoja,* hivyo kuukilia kiambatizi katika kitenzi husika kurejelea umoja pia.

Tofauti na uambatizi, unyambulishi huhusisha uundaji wa leksimu mpya. Vinyambulishi huleta mabadiliko ya maana rejezi au kategoria ya neno la awali (Bauer, 1988; Spencer, 1991; Katamba, 1993; Kiango, 2000). Mathalani, tukitumia kitenzi cha Kishambala '*shezigha*' (cheza), tunaweza kuunda leksimu '*mshezigho*' kwa kutumia kinyambulishi -*o*. Mchakato huu umebadili kabisa kategoria ya neno kutoka kitenzi kuwa nomino.

Katika makala hii, tutahusika na vipengele vifuatavyo vya uambatizi vya vitenzi: dhamira, njeo, hali, upatanishi, na urejeshi. Baadhi ya vipengele hivi vilichambuliwa na Besha (1985), aliyechunguza kwa undani njeo na hali. Data itakayotumika imetokana na ujuzi wa mwandishi ambaye ni msemaji wa Kishambala ikiwa lugha yake ya awali. Kutokana na kuwepo na lahaja kadhaa za Kishambala, lahaja ya Lushoto ndiyo itatumika katika uchambuzi huu. Lahaja hii hutofautiana na ile ya Mlalo, kama inavyoonyeshwa hapa chini:

1.

| **Mlalo** | **Lushoto/Korogwe** | |
|---|---|---|
| (a) *ingila* | *ingia/ingiya* | Ingia |
| (b) *lawa* | *Awa* | Toka |
| (c) *tongela* | *Tongea* | Fuata |

Kwa kutumia mifano 1(a), (b) na (c), tunaona utofauti wa kifonolojia kati ya lahaja ya Mlalo na ile ya Lushoto/Korogwe. Mara nyingi Lushoto/Korogwe, fonimu /l/ inapojitokeza hudondoshwa na irabu inayobaki husimama pekee au wakati mwingine kama irabu iliyotangulia ni /i/, fonimu /y/ huchopekwa baada ya irabu hiyo. Kwa mfano neno *ingila* linavyobadilika na kuwa *ingia/ ingiya.* [1]

## 2.0 Uambatizi katika vitenzi vya Kishambala

### 2.1 Dhamira

Dhamira ni kipengee kimojawapo cha kisarufi ambacho huhusu uchanuzi wa nia mbalimbali katika kitenzi. Nia hizi hubainisha lengo la msemaji, mathalani, kutoa taarifa, kuamuru, kusihi au kukataa. Kiambishi -*e* katika Kishambala huonesha dhamira amrishi. Kiambishi hiki huambikwa baada ya viambishi vya nafsi na mzizi wa kitenzi. Hoja hii inashadidiwa na mfano ufuatao:

---

[1] Kwa ufafanuzi zaidi angalia Besha, (1985).

2.

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1 | *ntaghe* 'niuze' | *titaghe* 'tuuze' |
| 2 | *utaghe* 'uuze' | *mtaghe* 'muuze' |
| 3 | *ataghe* 'auze' | *wataghe* 'wauze' |

Irabu *-e* hutumika pia kuamrisha katika vitenzi kanushi. Huambikwa kwenye vitenzi vyenye viambishi kanushi na vya nafsi. Kwa mfano:

3.

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1 | *senghooke* 'sitasimama' | *ketighooke* 'hatutasimama' |
| 2 | *keughooke* 'hutasimama | *kemghooke* 'hamtasimama' |
| 3 | *keaghooke* 'hatasimama' | *kewaghooke* 'hawatasimama' |

Irabu nyingine inayoonesha dhamira amrishi ni *-a*. Irabu hii hupachikwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi bila kuambika viambishi vyovyote kabla ya mzizi. Mfano ufuatao unaonesha matumizi ya irabu amrishi *-a* katika Kishambala:

4.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| *uya* 'rudi' | *uyai* 'rudini' |
| *asha* 'tupa' | *ashai* 'tupeni' |
| *onda* 'tafuta' | *ondai* 'tafuteni' |

## 2.2 Njeo

Vitenzi vya lugha za Kibantu huambikwa viambishi njeo kubainisha wakati uliopo, uliopita na ujao. Katika Kishambala, njeo pia hubainishwa katika wakati uliopita, uliopo na ujao.

### *2.2.1 Njeo iliyopita*

Wakati uliopita hubainishwa na maumbo; *-te-*, *-iye* na *-za-*. Umbo *-te-* hudokeza kuwa tendo limefanywa dakika chache zilizopita. Maumbo *-iye* na *-za-* hudokeza kuwa tendo tajwa lilishafanyika muda kitambo, k.m. jana na juzi. Ifuatayo ni mifano michache ya utumizi wa maumbo hayo kwa kutumia kitenzi *tagha* 'uza':

5.

(a) *Ti-te-tagha matagi* 'Tu-njeo-uza mayai'.
(b) *Ti-tagh-iye matagi* 'Tu-uza-njeo mayai'.
(c) *Ti-za-tagha matagi* 'Tu-njeo-uza mayai'.

Maumbo *-te-* na *-za-* hayabadiliki katika mazingira yote kama inavyobainishwa katika 6 (a) na (b) katika data ifuatayo:

6.

| 'a' | 'b' | 'c' |
|---|---|---|
| ***ti-te-shezigha*** 'tu-li-cheza' | ***ti-za-shezigha*** 'tu-li-cheza' | [5]***ti-shezigh-e*** 'tulicheza' |
| ***ti-te-dika*** 'tu-li-pika' | ***ti-za-dika*** 'tu-li-pika' | ***ti-dik-iye*** 'tulipika' |
| ***ti-te-zughua*** 'tu-li-fungua' | ***ti-za-zughua*** 'tu-li-fungua' | ***ti-zughu-e*** 'tulifungua' |
| ***ti-te-itanga*** 'tu-li-ita' | ***ti-za-itanga*** 'tu-li-ita' | ***ti-itang-e*** 'tuliita' |
| ***ti-te-haghia*** 'tu-li-fagia' | ***ti-za-haghia*** 'tu-li-fagia' | ***ti-haghi-e*** 'tulifagia' |
| ***ti-te-ghooka*** 'tu-li-simama' | ***ti-za-ghooka*** 'tu-li-simama' | ***ti-ghook-e*** 'tulisimama' |
| ***ti-te-onda*** 'tu-li-tafuta' | ***ti-za-onda*** 'tu-li-tafuta' | ***ti-ond-iye*** 'tulitafuta' |
| ***ti-te-jata*** 'tu-li-tembea' | ***ti-za-jata*** 'tu-li-tembea' | ***ti-jat-iye*** 'tulitembea' |
| ***ti-te-awa*** 'tu-li-toka' | ***ti-za-awa*** 'tu-li-toka' | ***ti-aw-iye*** 'tulitoka' |
| ***ti-te-shizia*** 'tu-li-siliba' | ti-za-shizia 'tu-li-siliba' | ***ti-shizi-e*** 'tulisiliba' |
| ***ti-te-aza*** 'tu-li-poteza' | ***ti-za-aza*** 'tu-li-poteza' | ***ti-az-ize*** 'tulipoteza' |
| ***ti-te-uza*** 'tu-li-rudisha' | ***ti-za-uza*** 'tu-li-rudisha' | ***ti-uz-ize*** 'tulirudisha' |
| ***ti-te-isha*** 'tu-li-chunga' | ***ti-za-isha*** 'tu-li-chunga' | ***ti-ish-ize*** 'tulichunga' |
| ***ti-te-gwisha*** 'tu-li-angusha' | ***ti-za-gwisha*** 'tu-li-angusha' | ***ti-gwish-ize*** 'tuliangusha' |
| ***ti-te-toza*** 'tu-li-shika' | ***ti-za-toza*** 'tu-li-shika' | ***ti-toz-ize*** 'tulishika' |
| ***ti-te-gosha*** 'tu-li-lala' | ***ti-za-gosha*** 'tu-li-lala' | ***ti-gosh-ize*** 'tulilala' |
| ***ti-te-ja*** 'tu-li-kula' | ***ti-te-ja*** 'tu-li-kula | ***ti-j-iye*** 'tulikula' |
| ***ti-te-gwa*** 'tu-li-anguka' | ***ti-za-gwa*** 'tu-li-anguka' | ***ti-gw-iye*** 'tulianguka' |
| ***ti-te-asha*** 'tu-li-tupa' | ***ti-za-asha*** 'tu-li-tupa' | ***ti-ash-ize*** 'tulitupa' |

Umbo *-iye* linaweza kujidhihirisha kama *-e* au *-ize* ketegemeana na mazingira. *-iye* hujitokeza katika mazingira ambapo shina la kitenzi limeundwa na silabi moja au mbili, kwa mfano mashina *onda, jata, awa, ja* na *gwa* katika 6(c). Umbo *-ize-* hujitokeza katika vitenzi vyenye viambishi vya hali ya utendeshi. Kwa mfano, kwa kutumia vitenzi *uya* 'rudi', *agha* 'potea', *gwa* 'anguka', na *kina* 'anguka'. Vitenzi hivi vikipitia mchakato wa utendeshi tunapata maumbo yafuatayo:

7.

| **Kitenzi** | **Utendeshi** | **njeo(-ize)** |
|---|---|---|
| *uya* | *uz-a* | *ti-uz-ize* |
| *agha* | *az-a* | *ti-az-ize* |
| *gwa* | *gw-ish-a* | *ti-gw-ish-ize* |
| *kina* | *kin-y-a* | *ti-kin-y-ize* |

[2] Katika data (c), maumbo -e, -iye na -ize hupachikwa baada ya mzizi wa kitenzi na kiambishi tamati -a hudondoshwa. Hivyo mpangilio wa viambishi vya vitenzi hivyo kuwa nafsi+mzizi+ki ambishinjeo.

Kutokana na vitenzi kuwa katika hali ya utendeshi, *-y-* iliyopo katika kiambishi njeo *-iye-* hubadilishana nafasi na *-z-* na kupata umbo *-ize*. Kwa vitenzi *uya* na *agha*, mchakato wa utendeshi huathiri mzizi pia. Mofimu ya mwisho wa mzizi hubadilishana nafasi na *-z-* ambayo hurejelea mofimu ya mzizi na utendeshi pia.Vipo baadhi ya vitenzi ambavyo havijapitia mchakato wa utendeshi lakini kutokana na asili ya utendeshi katika vitenzi hivyo, hupokea umbo *-ize* pia. Tukitumia kitenzi *isha* 'chunga' kama mfano, kitenzi hiki hudokeza hali ya kukifanya kiumbe hai kile, hasa mifugo k.v ng'ombe, mbuzi n.k. Kutokana na kuwepo kwa hali ya utendeshi katika kitenzi hiki, kitenzi *ti-ish-ize* kuundwa.

Vipo vitenzi vingine ambavyo havioneshi hali yoyote ya usababishi, kama vile, *gosha* 'lala', *toza* 'shika', na *asha* 'tupa'. Vitenzi hivi mizizi yake inaishia na viambishi ambavyo vinashabihiana na vitenzi sababishi vya Kishambala. Ushabihiano huu hupelekea vitenzi hivi kupokea umbo *-ize* kuonesha wakati uliopita kama vitenzi hivyo vinavyoonekana katika 6(c). Mazungumzo yafuatayo yanaonesha utumizi wa *-te-*, *-za-* na *-iye-* katika mazingira halisi:

8.

**A**: *Kwai m(u)**za**ighawa kwa Zumbe zuzi?* 'Kwa nini mulipelekwa kwa Mjumbe juzi?'.

**B**: *Ti**te**gwiwa taaghua manga* 'Tulikamatwa tunachukua mihogo'.

**A**: *Kwai m(u)**za**ghua izo manga?* 'Kwa nini mulichukua hiyo mihogo?'

**B**: *Ti**te**iva saa. Mia tighu**iye** mbii du* 'Tulisikia njaa. Lakini tulichukua miwili tu'.

**C**: *Hata ati ni mbii du mia m(u)**te**bawa* 'Hata kama ni miwili tu lakini muliiba'.

Wakati mwingine, umbo *-a-* hutumika kurejelea wakati uliopita pia. Hebu tumakinikie sentensi zifuatazo:

9.

(a) *Ta-**a**-dughana mshi mng'we.* 'Tulikutana siku moja'

(b) *Ta-**a**-ja viogwe uja mshi.* 'Tulikula viazi vitamu siku ile'

Maneno kama *mshi mng'we* 'siku moja' na *uja mshi* 'siku ile' hufuata baada ya kitenzi kuonesha ukitambo wa tendo na kutokewepo kwa umahususi/ ubayana wa kufanyika kwa tendo hilo. Hata hivyo, kiambishi njeo hiki hutumika kwa nadra kwani kinashabihiana na umbo mojawapo linalorejelea wakati uliopo.

*2.2.2 Njeo iliyopo*

Maumbo yanayobainisha wakati uliopo katika Kishambala hujibainisha kama ifuatavyo:

10.

(a) *na-**a**-shenga swii.* 'ni-na-kata nywele'

(b) *n(i)-**ta**-shenga swii.* 'ni-na-kata nywele'

(c) *n(i) ø-shenga swi.i* 'na-kata nywele'

Katika 10 (a) na (b), maumbo *-a-* na *-ta-* huonesha kuwa tendo la kukata nywele linafanyika. Katika (c), hakuna umbo dhahiri linalooonesha kufanyika kwa tendo. Muundo huu hutumika zaidi kujibu maswali kama inavyodhihirishwa katika mifano ifuatayo:

11.

| **Swali** | **Jibu** |
|---|---|
| *Ushengai?* 'Unakata nini?' | *Nshenga swii* 'Nakata nywele' |
| *Ajai?* 'Anakula nini?' | *Aja viogwe* 'Anakula viazi vitamu' |
| *Waikaa hii?* 'Wanakaa wapi?' | Waikaa Usoto 'Wanakaa Lushoto' |

*2.2.3 Njeo ijayo*

Umbo linalobainisha wakati ujao katika Kishambala ni *-ne-*. Hebu tuone utumizi wa umbo hili kwa kutumia shina la kitenzi *ghula* 'nunua':

12.

| **Nafsi** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| 1 | ***ne**-n'i'-ghule* 'njeo-nafsi-mzizi-e' | ***ne**-ti-ghul-e* 'njeo-nafsi-mzizi-e' |
| 2 | ***ne**-u-ghule* 'njeo-nafsi-mzizi-e' | ***ne**-m-ghul-e* 'njeo-nafsi-mzizi-e' |
| 3 | ***ne**-a-ghul-e* 'njeo-nafsi-mzizi-e' | ***ne**-wa-ghul-e* 'njeo-nafsi-mzizi-e' |

Tofauti na wakati uliopita na uliopo, umbo la wakati ujao huchukua nafasi ya kwanza katika kitenzi. Umbo hilo hufuatiwa na viambishi nafsi, kisha kiambishi tamati *-a* hubadilika na kuwa *-e*. Mifano mingine ni k.m. *ne-ti-haghi-e* 'tutafagia', *ne-ti-j-e* 'tutakula', *ne-wa-uze* 'watarudisha'.

## 2.3 Hali

Hali ni kipengee cha kisarufi ambacho huonesha hadhi ya tendo husika. Hali na njeo huhusiana sana hata wakati mwingine kuwa vigumu kutofautisha vipengele hivi. Kutokana na ukaribu huo, mara nyingi viambishi hali hupachikwa sehemu ileile ambapo viambishi njeo hupachikwa. Katika Kishambala, hali timilifu, isotimilifu, masharti na endelevu hubainishwa kwa kutumia mofimu *-i-*, *-ke-*, *-ki-* na *-ku-*.

Mofimu -*i*- huonesha utimilifu wa tendo. Mofimu hii huambatana na mofimu ya wakati uliopita -*iye*- ambayo hupachikwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi. Mifano ifuatayo inaonesha utumizi wa mofimu hiyo:

13.
(a) *Ngw'ana a-**i**-j-iye nkande* 'mtoto ameshakula chakula'.
(b) *Tate a-**i**-iz-iye- pee* 'baba ameshakuja tayari'
(c) *Maghoto ya-**i**-aw-iye se* 'kondoo wameshatoka nje'.

Mofimu -*ke*- hubainisha hali isotimilifu. Tendo tajwa linaendelea wakati tamko linapotolewa. Mofimu hii hupachikwa baada ya kipatanishi, kisha kufuatiwa na mzizi wa kitenzi. Hakuna umbo njeo lolote linaloambatanishwa kama mifano ifuatayo inavyoonesha:

14.
(a) *Ongoai ishwi ti-**ke**-haka* 'tangulieni sisi bado tunaoga'.
(b) *Ghoto ji-**ke**-ja mani* 'kondoo bado anakula majani'.

Kiambishi -*ki*- huonesha hali ya masharti. Kiambishi hiki huambikwa baada ya kiambishi nafsi, kisha kufuatiwa na shina la kitenzi kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

15.
(a) *N(i)-**ki**-daha neniize* 'nikiweza nitakuja'.
(b) *A-**ki**-j-a manga neaungw'e ni ifu* 'akila mihogo ataumwa na tumbo'.
(c) *Wa-**ki**-kunda newaime* 'wakipenda watalima'.

Katika 15 (a), (b) na (c), inaonekana kuwa utekelezaji wa matendo ya pili lazima yatanguliwe ya matendo yaliyotajwa mwanzo. Mathalani katika 16 (b), lazima mhusika ale mihogo kwanza ndio tumbo limuume na asipokula basi tendo la kuumwa tumbo halitatimia.

Kiambishi *ku*- katika Kishambala hudokeza tendo lisiloukomo. Hakibadili maana rejezi au kategoria ya vitenzi vilivyoorodheshwa katika namba 16, bali hutaarifu tu kuwa tendo husika ni endelevu.

16.
(a) ***ku**shenga* 'kukata'
(b) ***ku**tagha* 'kuuza'
(c) ***ku**ng'ooka* 'kukimbia'
(d) ***ku**ghooka* 'kusimama'
(e) ***ku**uya* 'kurudi'

## 2.4 Upatanishi

Baadhi ya viambishi vinavyopachikwa katika vitenzi hubainisha kiima au yambwa. Viambishi hivi huhusu *upatanishi* wa kisarufi kutegemeana na nomino husika katika sentensi. Mfumo wa ngeli wa Kishambala hautofautiani na mifumo mingine katika lugha nyingine za Kibantu; hapa tutatoa mifano michache ya viambishi vya kiima na yambwa kwa kutumia ngeli za nomino M-/MA-, M-/MI-, na Ø-/MA-[3]. Tutaanza na mifano ya viambishi vya kiima.

17.

(a) **Ngeli ya** M-/WA-, **vipatanishi** ni *na-/ta-* (nafsi ya kwanza), *wa-/mwa-* (nafsi ya pili) na *a-/wa-* (nafsi ya tatu).

**Mifano:**

*Imi **na**aonda hantu ha kugosha/Ishwi **ta**aonda hantu ha kugosha.*
'Mimi ninatafuta mahali pa kulala/Sisi tunatafuta mahali pa kulala'.
Iwe ***wa**aonda hantu ha kugosha/Inywi **mwa**aonda hantu ha kugosha.*
'Wewe unatafuta mahali pa kulala/Ninyi mnatafuta mahali pa kulala'.
*Ye **a**aonda hantu ha kugosha/ Wo **wa**aonda hantu ha kugosha.*
'Yeye anatafuta mahali pa kulala/ Wao wanatafuta mahali pa kulala'.

(b) **Ngeli ya** M-/MI-, **vipatanishi** ni *u-/i-*.

**Mifano:**

***Mz**itu **u**zashengwa woshe.*
Msitu umekatwa wote.
***Mi**zitu **i**zashengwa yoshe.*
Misitu imekatwa yote.

(c) **Ngeli ya** Ø-/MA- , **kipatanishi** ni *ya-*.

**Mfano:**

***Ma**zi **ya**zaitika.*
Maji yamemwagika.

Viambatizi vinavyorejelea yambwa huukiliwa pia na kategoria ya nomino tangulizi. Hebu tuone mifano ifuatayo kwa kutumia kategoria zilezile zilizotumika katika 17 (a) na (b).

---

[3]Kuhusu ufafanuzi wa ngeli za nomino za Kishambala, angalia Besha (1985).

18.

(a) **Ngeli ya** M-/WA-, **vipatanishi** ni *-ni-/-ti-* (nafsi ya kwanza), *-ku-/-mi-* (nafsi ya pili) na *-mu-/-wa-* (nafsi ya tatu).

**Mifano:**

*Mame aa**ni**ondea mbogha/Mame aa**ti**ondea mbogha.*
'Mama ananitafutia mboga/Mama anatutafutia mboga'
*Mame aa**ku**ondea mbogha/Mame aa**mi**ondea mbogha.*
'Mama anakutafutia mboga/Mama anawatafutia mboga'
*Mame aa**mu**ondea mbogha/Mame aa**wa**ondea mbogha.*
'Mama anamtafutia mboga/Mama anawatafutia mboga'

(b) **Ngeli Ngeli** ya M-/MI-, **vipatanishi** ni *-u-/-i-*.

**Mfano:**

***M**tumba aa**u**shenga uja mti/Mtumba aa**i**shenga ija miti.*
'Mjomba anaukata ule mti/ Mjomba anaikata ile miti'

Viambatizi vya kiima huchukua nafasi ya kwanza katika kitenzi kama inavyojikeza katika 17, wakati ambapo viambatizi tendewa hupachikwa kabla ya mzizi kama inavyobainishwa katika 18.

## 2.5 Urejeshi

Viambishi rejeshi katika Kishambala huukiliwa pia na ngeli za nomino. Hebu tuone mifano kwa kutumia baadhi ya kategoria za nomino (MU-/WA-, M(U)-/MI, Ø-/ MA, KI-/VI-, N-/N-) kati ya zile zilizoainishwa na Besha (1985).

19.

| 'a' **MU-/WA-** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Nafsi** | **Umoja** | | **Wingi** | |
| 1 | *n'i'-sheng-iye-**ye*** | 'niliyekata' | *ti-sheng-iye-**wo*** | ' tuliokata' |
| 2 | *u-sheng-iye-**ye*** | 'uliyekata' | *m'u'-sheng-iye-**wo*** | 'muliokata' |
| 3 | *a-sheng-iye-ye* | 'aliyekata' | *wa-sheng-iye-**wo*** | 'waliokata' |

| 'b' **M'U'-/MI-** | |
|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** |
| *Mti u-kin-iye-**wo*** 'Mti ulioanguka' | *Miti i-kin-iye-**yo*** 'Miti iliyoanguka' |

| 'c' **Ø-/ MA-** | |
|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** |
| *Mazi ya-itik-e-**yo*** 'Maji yaliyomwagika' | - |

| 'd' **KI-/VI-** | |
|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** |
| *Kintu chi-banik-e-**cho*** 'Kitu kilichoharibika' | *Vintu vi-banik-e-**vyo*** 'Vitu vilivyoharibika' |


| 'd' **KI-/VI-** | |
|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** |
| *Kintu chi-banik-e-**cho*** 'Kitu kilichoharibika' | *Vintu vi-banik-e-**vyo*** 'Vitu vilivyoharibika' |


| 'e' **N-/N-** | |
|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** |
| *Shuke i-tatuk-e-**yo*** 'Nguo iliyochanika' | *Shuke zi-tatuk-e-**zo*** 'Nguo zilizochanika' |

Kwa kutumia mifano katika 19, maumbo rejeshi katika vitenzi vya Kishambala ni *-e* na *-o*. Maumbo haya huweza kuchukuliwa kama mizizi ambapo vipatanishi huambikwa kabla na kupata maumbo k.m. *-ye*,*-wo*, *-cho* n.k. Hata hivyo, umbo *-e* hujitokeza katika kategoria ya MU-/WA- tu. *-y* hupachikwa kabla ya *-e* na kupata umbo rejeshi *-ye* kwa nafsi zote tatu, katika umoja. Katika kategoria nyingine za nomino zilizobaki, vipatanishi hupachikwa kabla ya *-o*. Mchakato huu hutuzalia maumbo ya ndani na baada ya utumizi wa kanuni mbalimbali za kimofofonolojia, tunapata maumbo ya nje, kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

20.

**MIFANO YA VIAMBISHI REJESHI VYA KISHAMBALA**

| Kategoria ya nomino | Vipatanishi | Umbo la ndani | Kanuni | **umbo la nje** |
|---|---|---|---|---|
| (a) M(U)-/WA- | a-[4] | - | - | -ye |
| | wa- | wa+o | Udondoshaji | -wo |
| (b) M(U)-/MI- | u- | u+o | Uyeyushaji | -wo |
| | i- | i+o | Uyeyushaji | -yo |
| (c) Ø-/ MA- | Ya- | ya+o | Udondoshaji | -yo |
| (d) KI-/VI- | chi- | chi+o | Udondoshaji | -vyo |
| | vi- | vi+o | Uyeyushaji | -cho |
| (e) N-/N- | i- | i+o | Uyeyushaji | -yo |
| | Zi- | zi+o | Udondoshaji | -zo |

[4]Kipatanishi hiki kinaweza kuchukuliwa kuwa ni kighairi kwani kinakinzana na vipatanishi vingine.

## 2.6 Hitimisho

Uambatizi wa vitenzi, hasa katika lugha za Kibantu kama Kishambala, hujumuisha vipengele vingi. Katika makala hii fupi, vipengele vilivyobainishwa ni njeo, hali, nafsi, dhamira, urejeshi na upatanishi. Vipengele hivi vipo katika mchakato wa uambatizi kwa sababu havibadili maana au kategoria ya neno, bali huongeza nduni za kisarufi tu katika vitenzi. Makala haikuhusika na kila kipengele; bali inawakilisha sehemu ndogo tu ya utafiti unaoendelea kuhusu sarufi ya Kishambala.

## Marejeo


Bauer, Laurie. (1988). *Introduction to Linguistics Morphology*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Besha, Ruth. M. (1985) *A Study of Tense and Aspect in Shambala* (Unpublished PhD Thesis) University of Dar es Salaam.

Katamba, Francis. (1993) *Morphology*. New York: St. Martin's Press.

Kiango, John Gongwe. (2000). *Bantu Lexicography: A Critical Survey of the Principles and Process of Constructing Dictionary Entries*. Tokyo: Fujiwara Printing Co. Ltd.

Spencer, A. (1991) *Morphological Theory*. Oxford: Blackwell.